**Mwandishi wa makala haya, Mashaka Mgeta akimhoji mwanamke anayetajwa kwa jina la Bhoke, aliyefanyiwa unyanyasaji kutokana na utasa.**

# Utasa unavyochochea unyanyasaji dhidi ya wanawake Tarime

**Mashaka Mgeta**

UNYANYASAJI wa kijinsia ni miongoni mwa kero kwenye jamii zinazowaathiri watu hususani wanawake, wasichana na watoto. Vitendo hivyo vinatokea sehemu mbalimbali duniani.

Nchini Tanzania, mikoa kadhaa inatajwa kupitia takwimu mbalimbali, kwamba inaongoza kwa vitendo hivyo, Mara ikiwa mmoja wapo.

Utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka 2015, ulionesha mkoa wa Mara uliongoza kwa asilimia 66.4 ya kuwapo kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vikiwamo vilivyofanywa dhidi ya wanawake wasiokuwa na uwezo wa kubeba ujauzito.

Mkurugenzi wa LHRC, Dk Kijo Bisimba akaitaja mikoa mingine na asilimia zake kwenye mabano kuwa ni Kagera (46.4) na Mwanza na Geita (43).

Ni rahisi zaidi kwa mwanaume asiyeweza kuzalisha kuishi katika hali hiyo kuliko mwanamke anayenyanyaswa kiasi cha kudhalilishwa utu na kupokonywa haki ya kufanya uamuzi wa kuchagua.

Bhoke Matiko, mwanamke aliyethibitika kutokuwa na uwezo wa kupata ujauzito, ni miongoni mwa maelfu ya wanawake wanaonyanyaswa na kubaguliwa kutokana na hali hiyo.

Mkoani Mara hususani katika wilaya ya Tarime, jamii ya kabila la Wakurya anapotokea Bhoke, wana desturi ya kuendeleza vitendo hivyo kwa namna tofauti; mosi kwa unyanyasaji na ubaguzi.

Pili ni kuruhusu ndoa za kimila za jinsia moja (wanawake) ili mwanamke 'anayeolewa' amzalie mtoto yule asiyekuwa na uwezo wa kubeba ujauzito; hii inajulikana kama 'nyumba ntobhu'. Nitaielezea baadaye.

Bhoke (si jina halisi kutokana na sababu za usalama wake) ni miongoni mwa wanawake ambao hawakujaliwa kupata kizazi.

Anasema jitihada za kutaka kupata ujauzito zilimfikisha maeneo tofauti ikiwamo kwa waganga wa asili na wahubiri wanaojitangaza kupitia vyombo vya habari kwamba wanaponya maradhi na kuwawezesha wahitaji kupata ujauzito.

Aliolewa akiwa na umri wa miaka 16 na kijana wa Kikurya anayemtaja kwa majina ya Wankyo Chacha, wote wakiwa wa ukoo wa Watimbaru na wakazi wa wilaya ya Tarime wanaoishi mjini Musoma

Kijiografia Tarime ni wilaya mojawapo mkoani Mara ambayo kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, idadi ya wakazi wa wilaya hiyo ilihesabiwa kuwa 339,693.

Kwa mujibu wa Bhoke, ni kawaida kwa msichana wa Kikurya kuolewa katika umri huo, hasa inapotokea kushindwa kuendelea na masomo ya sekondari.

Lakini pia vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa (CAP 29 R.E 2002) inaruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 kwa kibali cha mahakama, na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi.

Bhoke anasema, "sikubahatika kuendelelea na masomo ya sekondari, hivyo kwa makubaliano na wazazi wangu, niliolewa na Wankyo akiwa mfanyabiashara ndogondogo mjini Musoma," anasema.

Anasema walifunga ndoa ya kimila wilayani Tarime mwaka 2000 na kuanza maisha ya mume na mke wakiwa wamepanga kwenye vyumba viwili mjini humo.

Kwa mujibu wa Bhoke, maisha hayo yaliwachukua takribani miaka saba walipojaliwa kujenga nyumba yao kwenye manispaa ya Musoma mwaka 2005, wakati huo akiwa hajapata ujauzito.

Licha ya uvumilivu na kushiriki shughuli za kukuza kipato cha familia, Bhoke anasema mwaka mmoja baada ya kuolewa, ndugu wa upande wake na wa mumewe walianza kuhoji ni kwa nini hajapata ujauzito.

UMUHIMU WA UJAUZITO

"Kwa sisi Wakurya mwanamke anapoolewa, tegemeo la kwanza la familia zote ni kupata mtoto, sasa mwaka mmoja ulipopita niliulizwa mara kadhaa, kwa nini sijapata ujauzito," anasema.

Wakati hali ikiwa hivyo, Bhoke anasema hata mumewe, Wankyo alikuwa akihoji mara kwa mara kwa nini hapati ujauzito na wakati mwingine kumuamuru akafundishwe kuhusu elimu ya uzazi kwa shangazi yake ili ayajue majira ya uzazi.

"Hata mume wangu hakufurahishwa mimi kutopata ujauzito, lakini ukweli ni kwamba nilijitahidi ila sikuona mafanikio, nilianza kumuuliza shangazi, akanipa mbinu tofauti zikiwamo za asili, lakini haikuwezekana," anasema.

Bhoke anasema baada ya kipindi hicho, alianza kuitwa majina ya kejeli kama 'mjaza choo' na 'mzigo' huku ndugu wa mumewe wakimshinikiza Wankyo (mumewe) aoe mke wa pili ili familia hiyo ijiepushe na upweke uliotokana na kutokuwa na mtoto.

Anasema aliitwa 'mjaza choo' na 'mzigo' ikimaanisha mtu anayekula pasipo kupata ujauzito na kuleta watoto kwenye familia.

Bhoke anasema wakiwa katika mwaka wa tano wa ndoa yao, mumewe, Wankyo alianza kumfanyia visa ikiwamo kulala kwa wanawake aliomtajia kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kwamba lengo lilikuwa ni kupata mtoto.

"Nilipojaribu kumuonya (Wankyo) niliambulia kipigo kufikia hatua ya kunijeruhi mkono wangu wa kushoto," anasema akionesha kovu linaloashiria jeraha alilopata kutokana na kipigo hicho.

Bhoke anasema mashauri yanayotokana na unyanyasaji huyo yanatatuliwa kwa mazungumzo ya familia za mume na mke na kwamba kuyafikisha

**INAENDELEA UK 17**

# Utasa unavyochochea unyanyasaji dhidi ya wanawake Tarime

**INATOKA UK 16**

kwenye vyombo vya sheria ni sawa na kuidhalilisha jamii ya Wakurya.

**KWENDA HOSPITALI**

Anasema ni kutokana na hali hiyo, alishauriwa na baadhi ya ndugu zake, amuombe mumewe kumpeleka hospitali ya mkoa wa Mara iliyopo katika manispaa ya Musoma ili akapimwe kujua chanzo cha tatizo hilo.

"Lengo hapa lilikuwa nikifika hospitalini hapo niongee na madaktari wampime na mume wangu ili tujue ikiwa tatizo linaweza kuwa upande wake," anasema na kuongeza kwamba vipimo vilibaini kwamba tatizo lipo kwake (Bhoke).

Bhoke anasema hali hiyo ilimfanya kuwa na wakati mgumu, ingawa alifarijiwa mara kwa mara na ndugu na rafiki zake huku upande wa mumewe wakiendeleza shinikizo kwa Wankyo ili aoe mke wa pili.

Kwa mila na desturi za Wakurya, mwanaume anaruhusiwa kwa wakati wowote na pasipo masharti, kuona idadi ya wanawake anayoona watamfaa katika kuijenga familia yake.

**APATA MKE MWENZA**

Hivyo, anasema mwaka 2006, Wankyo alioa mke wa pili (anamtaja jina) pasipo kumtaliki. Anasema mke huyo wa pili aliolewa akiwa mjamzito, hivyo ilimchukua takribani miezi saba, akajifungua.

Anasema kujifungua kwa mwanamke huyo kulizidisha mapenzi ya Wankyo na ndugu zake kwa mke huyo wa pili, na mara kadhaa alimtamkia (Bhoke) kwamba atabaki kuwa mwanamke wa kumfurahisha kimwili tu.

Ilimpasa kudumu katika hali hiyo kwa sababu za kimila, kwamba mwanamke wa Kikurya akiolewa hapaswi kuachika pasipo ridhaa ya mumewe, na kwamba endapo itakuwa kinyume chake familia ya mwanamke itarejesha mahari iliyotolewa.

Kwa Bhoke, wazazi wake walipokea mahari ya ng'ombe 12 na mbuzi wanne, mifugo ambayo kwa wakati huo isingekuwa rahisi kurejeshwa kwa vile ingekuwa fedheha kwa familia na ilishakuwa katika milki ya familia.

Hata hivyo, siku chache baada ya Machel kuondoka wilayani Tarime, ikaripotiwa kwamba mwanamke Anna (18) alikatwa kwa mapanga na mumewe aliyetajwa kwa jina moja la Weghai kwa sababu ya kuchelewa kushika ujauzito.

Tukio hilo lilitokea katika kijiji cha Mariba wilayani humo, wakati wawili hao katika mwaka wa pili tangu Februari mwaka jana walipoanza kuishi pamoja wakiwa mume na mke.

Anna aliyeshonwa nyuzi 67 baada ya kujeruhiwa kwenye bega la kushoto, akaelezea kufanyiwa unyanysaji na mateso katika ndoa yake, vikiwamo vipigo vya mara kwa mara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Valeria Msoka-kwa wakati huo, akazungumzia tukio hilo na kulitaja kuwa moja ya matukio ya ukatili uliovuka mipaka, lakini akasisitiza asasi yake na nyingine za kupinga unyanyasaji wa kijinsia zitaendeleza jitihada za kupambana na matukio ya namna hiyo katika jamii.

Mkurugenzi wa Wakfu wa Graça Machel, Graça Machel akizungumza na wasichana wilayani Tarime.

Mwanamke anna John aliyekatwa kwa panga kutokana na kuchelewa kupata ujauzito.

**UTHIBITISHO WA 'NYUMBA NTOBHU'**

Chacha Machugu (75) ni mmoja wa wazee wa Kikurya, anathibitisha kuwa kujifungua mtoto ni moja ya sifa ya mwanamke kubaki kwenye ndoa, na kwamba kinyume chake anapaswa kuachika.

"Kama mwanamke hapati ujauzito ataishi vipi kwenye familia," anahoji Machugu na kusema miongoni mwa mbinu za kimila zinazotumika ni kumtaliki mwanamke tasa na kumsaidia kuoa msichana kwa ndoa inayotambulika kama 'nyumba nthobhu'.

`Nyumba ntobhu' ni neno la Kikurya linalomaanisha 'familia dhaifu' kutokana na ukweli kwamba mkuu wake ni mwanamke.

Mwanamke tasa ndiye anayeona msichana na ana mamlaka ya kumchagulia mume ama wanaume wa kushiriki naye tendo la ndoa, ili apate ujauzito na kujifungua watoto wanaotambulika kuwa wake (mwanamke tasa).

Nyambura Werema (68) ni mwanamke tasa mkaazi wa wilayani Tarime anayemiliki 'nyumba ntobhu' anasema mabadiliko ya fikra za watu na maendeleo yaliyopo ni miongoni mwa sababu zinazoifanya desturi hiyo kuonekana isiyofaa.

"Mimi wakati ninamuoa mama aliyenizalia hawa watoto watatu zaidi ya miaka 40 iliyopita, ilikuwa ni jambo la heshima kwetu, lakini sasa ukitaja 'nyumba ntobhu' inakuwa fedheha na wanawake wanadhalilika," anasema.

**HITAJI LA UELIMISHAJI**

Silvanus Mgomba ni mmoja wa waelimishaji rika katika taasisi ya Save your Generation Tanzania (SAGETA), aliyewahi kushiriki miradi ya hamasa kuhusu uzazi wa mpango mkoani Mara.

Anasema utasa ni hali inayoweza kumpata mwanamke nje ya matarajio yake, lakini kinachotakiwa ni kuzidisha elimu kwa jamii itakayofanikisha kuondokana na vitendo vya ubaguzi na unyanyasaji dhidi yao. Hivi karibuni, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Glorious Luoga, alizitaka mamlaka za Serikali wilayani humo kuwamakata wahusika wa vitendo vinavyoashiria kumnyanyasa mwanamke, ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili wahusika waadhibiwe na kuwa fundisho kwa wengine.

Mkurugenzi wa Wakfu wa Graça Machel, Graça Machel, anatoa tumaini jema kwa wanawake na wasichana wanaonyanyaswa kwa namna tofauti wilayani Tarime, akisema hawapaswi kukata tamaa wakati jitihada za kuondokana na kadhia hiyo zikifanywa na wadau tofauti ikiwamo Serikali.

Machel aliyefanya ziara wilayani humo hivi karibuni akasema unyanyasaji unaofanyika kwa kada hiyo ni pamoja na unaotokea kwenye ndoa, mahusiano ya ngono na mashambulizi ya kimwili.

Mwaka jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ushirika wa Kutokomeza Ukeketaji (ATFGM) cha Kanisa Katoliki, Sista Stelle Mgaya alieleza kupokea wanawake 3,000 kati ya 5,000 wanaojulikana kuathirika kwa vitendo vya unyanyasaji wilayani humo.

Kwa hali hiyo, ni dhahiri kwamba nafasi ya utasa inachangia kushamiri kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, hivyo uwekezaji katika kuielimisha jamii iepukane na vintendo hivyo na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wanawake wasiokuwa na uwezo wa kubeba ujauzito ili wasifedheheke.

+255754691540